

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA



27/04/2022

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA

- Msimamizi wa Uchaguzi Halmashauri ya Wilaya ya Siha kwa kuzingatia Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za Mwaka 2019 na Tangazo la Serikali namba 373, anakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi ishirini na nne (24) za Waandikishaji wa Orodha ya Wapiga Kura kwa ajili ya Uchaguzi mdogo wa **Wenyeviti wa Vijiji vya Ngumbaru, Mendai, Olkolili, Mae Juu, Munge na Mlangoni na Wenyeviti wa Vitongoji vya Mawasiliano, Donyomurwak, Oloiwang, Megwara, Isabilony, Kishofu Laktore, Darajani na Mkombozi A.**

A. SIFA ZA MWOMBAJI.

- Awe ni raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi.
- Awe amemaliza elimu ya kidato cha nne (4) au zaidi, anayeweza kusoma na kuandika vizuri, na anayeweza kuyaelewa maelekezo kwa Waandikishaji wa orodha ya Wapiga Kura.
- Asiwe shabiki au Kiongozi wa Chama cha Siasa.
- Awe Mwadilifu, Mtiifu na mwenye akili timamu.
- Awe mkazi wa Kijiji ambacho anaomba nafasi hiyo.
- Anapoandika barua ya maombi ataje Kata, Kijiji na Kitongoji anachotoka

B. MASHARTI YA JUMLA

- Waombaji waambatishe maelezo binafsi (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (Referees) wawili.

- Maombi yote yaambatane na Vyeti vya Taaluma, nakala za Vyeti vya Kidato cha Nne, Kidato cha Sita au kuhitimu mafunzo kwa kuzingatia sifa kwa mujibu wa Tangazo hili.
- Waombaji waambatishe picha mbili 'Passport size' za hivi karibuni.
- Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma wapitishwe barua zao za maombi ya nafasi ya kazi kwa Wakuu wa Taasisi zao na kwa wale ambao sio Watumishi wapitishwe kwa Watendaji wa Kata wanazotoka.
- Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kughushi watachukuliwa hatua za kisheria
- Maombi yote yawasilishwe katika Ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi Halmashauri ya Wilaya ya Siha.
- **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 04 Mei , 2022 saa 9:30 Alasiri**

Anuani ya kutuma maombi ya kazi ni:-

Msimamizi wa Uchaguzi,
Halmashauri ya Wilaya ya Siha,
S.L.P 129,
SIHA.

Imetolewa na:-



Mangali U. E

**MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**

